



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**



TAARIFA KWA UMMA

**WATAHINIWA 948 KUFANYA MTHANI WA KIDATO CHA SITA 2025
ILEMELA**

Katika mwaka 2025, jumla ya watahiniwa **948** waliosajiliwa kufanya mthani wa kidato cha sita katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela wanatarajia kuanza mthani huo utakaofanyika kuanzia tarehe **05 hadi 26 mwezi Mei mwaka 2025**.

Kati ya watahiniwa hao 948, **wavulana ni 235 na wasichana ni 713** ambapo watahiniwa wa shule (**S**) wapo **919** (wasichana wakiwa **702** na wavulana wakiwa **217**), watahiniwa **13** ni wa kujitegemea (**PC**) wote wakiwa wavulana na watahiniwa wa ualimu (**CHUO**) ni **16** (wavulana **5** na wasichana **11**).

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Bi. **Ummu Wayayu**, kwa niaba ya uongozi wa Ilemela anawaomba na kuwatakia kila la kheri watahiniwa wote wa Ilemela watakaofanya mthani huo wa kidato cha sita 2025, aidha amewataka kujiepusha na tabia zozote za udanganyifu zitakazopelekea kufutiwa mthani na amewakumbusha kuzingatia na kufuata taratibu zote za mitihani ili waweze kuhitimu mitihani yao salama.

Manispaa ya Ilemela ina jumla ya vituo **10** vya kufanyia mthani ambapo vituo **8** ni vya watahiniwa wa shule, kituo kimoja ni cha watahiniwa wa kujitegemea na kituo kimoja ni cha watahiniwa wa ualimu (**chuo**).

Violencea S. Mbakile
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela
02/05/2025

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, 200 BR.ya Buswelu,33282
Buswelu Ilemela Mwanza, S.L.P 735 BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz, Tovuti: www.ilemelamc.go.tz